

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA HAMSINI NA NNE

26 JUNI, 2024



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA HAMSINI NA NNE – TAREHE 26 JUNI, 2024

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**692. MHESHIMIWA HASSAN ZIDADU KUNGU
(TUNDURU KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna upungufu kiasi gani wa Walimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru na upi mpango wa kuondoa upungufu huo.

693. MHESHIMIWA GRACE VICTOR TENDEGA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutenga Fedha ili kuweka uwiano sawa katika Bajeti za Halmashauri ambazo zinasaidia katika ujenzi wa Vituo vya Afya.

OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):

694. MHESHIMIWA SAASHISHA ELINIKYO MAFUWE (HAI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kunakuwa na Mpango wa Maendeleo walau wa miaka 50 pamoja na kuwa na vipaumbele vya Taifa.

WIZARA YA NISHATI:

695. MHESHIMIWA JOSEPH ZACHARIUS KAMONGA (LUDEWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini changamoto za bei na mgao wa umeme Kata za Mawengi, Lubonde, Lugarawa, Lupanga, Mlangali, Madilu, Milo na Mawengi zitamalizika.

696. MHESHIMIWA FLATEI GREGORY MASSAY (MBULU VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itakamilisha usambazaji wa Umeme wa REA katika Kata na Vijiji 23 vya Jimbo la Mbulu Vijijini.

WIZARA YA UJENZI:

697. MHESHIMIWA SUMA IKENDA FYANDOMO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini ujenzi wa Barabara ya Njia Nne kutoka Igawa hadi Tunduma utakamilika.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

698. MHESHIMIWA MICHAEL COSTANTINO MWAKAMO (KIBAHA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itaipatia vitendea kazi kama Magari, Majengo na Shajala Wilaya ya Kipolisi ya Mlandizi Jimbo la Kibaha Vijijini.

699. MHESHIMIWA JAFARI WAMBURA CHEGE (RORYA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kudhibiti wahalifu wanaowavamia Wavuvi wakiwa Ziwani na kuwanyang'anya mali zao.

700. MHESHIMIWA NDAISABA GEORGE RUHORO (NGARA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itatatia mgogoro wa Ardhi kati ya Gereza la Rusumo na Wananchi wa Kijiji cha Rusumo.

WIZARA YA MAJI:

701. MHESHIMIWA MOHAMED LUJUO MONNI (CHEMBA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itafanya ukarabati wa miundombinu ya maji iliyochakaa na kusababisha upungufu wa maji - Chemba.

702. MHESHIMIWA BONIPHACE MWITA GETERE (BUNDA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini mradi wa maji ya Ziwa Victoria kutoka Butiama kwenda Nyamuswa - Bunda utakamilika.

703. MHESHIMIWA MRISHO MASHAKA GAMBO (ARUSHA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Mradi wa Majitaka uliopo Kata ya Olmot ambao utaunganishwa na Kiwanda cha A to Z utakamilika.

WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:

704. MHESHIMIWA HUSNA JUMA SEKIBOKO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kusimamia ipasavyo Biashara za Mitandaoni nchini.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

705. MHESHIMIWA NEEMA WILLIAM MGAYA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini Serikali itamaliza mgogoro wa mpaka kati ya Hifadhi ya Mpanga Kipengele na Vijiji vya Luduga, Mpanga, Malangali na Wangamiko.

III. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2023 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

WAZIRI WA FEDHA:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

(Majadiliano yanaendelea)

IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

(Kusomwa kwa Hatua zake zote)

Muswada wa Sheria ya Fedha za Matumizi wa Mwaka 2024 (*The Appropriation Bill, 2024*).

DODOMA
26 JUNI, 2024

N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE